HABARI LEO UK 18.

# Watendaji wabanwa migogoro ya wakulima, wafugaji



Na Mwandishi Maalumu, Kilwa

MKUU wa Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi, Zainabu Kawawa (pichani) ametoa mwezi mmoja kwa watendaji na madiwani wa halmashauri hiyo kujitathmini juu ya ongezeko la migogoro ya wafugaji na wakulima inayotokea maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Akizungumza katika baraza la madiwani, Zainabu alisema alishatoa maagizo ambayo yalistahili kuzingatiwa na watendaji ili kuepusha migogoro isiyokuwa na tija, lakini hali bado inaendelea.

Alisema katika mazingira ya sasa hatakubali kuendelea kuwepo kwa migogoro hiyo inayosababishwa na utendaji dhaifu wa viongozi katika ngazi za chini wanaokiuka misingi ya utumishi wa umma.

Zainabu aliagiza kuundwa kwa kamati ya maridhiano kati ya wakulima na wafugaji na kuangalia idadi ya mifugo iliyopo katika kila kata na kupewa taarifa, lakini mpaka sasa ni kata tano tu kati ya 23 zilizopeleka taarifa ya mifugo.

Aidha, katika mkutano huo alisema haridhiki na kutotekelezwa kwa agizo la kupelekwa kwa mifugo iliyosajiliwa Kilwa katika maeneo ya wafugaji na kusema idadi ya sasa ya mifugo haikubaliki wilayani humo.

Zainabu pia alisema hakuna utekelezaji uliofanyika kuhusu agizo lake la kusajili mifugo na wafugaji kupelekwa katika maeneo yaliyotengwa pamoja na ulazima wa kuchimba mabwawa ya kunyweshea mifugo ili kuepuka mwingiliano wa mifugo na maeneo ya kilimo.

Alisema kutotekelezwa kwa maagizo yake kunaleta matatizo kwa wananchi na akaonya kwamba hatavumilia.

"Nawapeni watendaji wote na wataalamu mwezi mmoja kujitathmini na kuondoa hii hali ya mateso kwa wananchi," alisema mkuu huyo wa wilaya.

Katika mahojiano baada ya kikao hicho, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kilwa, Eston Ngilangwa alisema amepokea maagizo ya mkuu wa wilaya na kuonya watendaji walio chini yake kuacha ubabaishaji na kutekeleza maagizo hayo.

"Tuna majina tumepewa ya watendaji wanaoshirikiana na wafugaji na kusababisha mtafaruku mkubwa kwa wakulima, umetolewa mwezi mmoja wasipobadilika nitawachukulia hatua," alionya Ngilangwa.

Alisema uvamizi wa wafugaji ni changamoto kubwa katika wilaya hiyo ambayo kwa sasa haiwezi kuendelea kuchukua zaidi wafugaji.

"Hawa ni Watanzania wenzetu, lakini sheria na taratibu lazima zifuatwe. Tutaanzisha operesheni kubwa ya walioingiza mifugo kinyemela bila taratibu tutawarudisha wanakotoka," alisema mkurugenzi.

Alisema watashirikiana na mamlaka nyingine katika kukabiliana na tatizo hilo hasa mamlaka zilizo na majeshi kama Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na polisi.

Alisema pamoja na wilaya kuzidiwa na mifugo lakini pia wafugaji wamekuwa hawaendi walikoelekezwa kukaa na mifugo yao kwani hata maeneo hayo nayo yamezidiwa na hivyo kusababisha ugomvi kati yao na wakulima.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kilwa, Farida Kikoleka alisema ipo haja ya kuwa na kikao kazi kati ya madiwani, mkuu wa wilaya na watendaji wa halmashauri kuona namna bora kabisa ya kukabiliana na uvamizi wa mifugo.

"Kilwa ina ng'ombe wengi kuliko idadi ya watu, ng'ombe wametosha," alisema Farida na kuongeza kuwa wakati umefika kwa wilaya hiyo kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji.

Diwani wa Kata ya Kandawale ambayo imeathirika sana na uvamizi huo, Hemed Kimbugu alisema wafugaji wanatumia jeuri ya fedha kuwakabili wananchi na pia hutumia nguvu na mikuki yao kuwafanya watu waogupe akitolea mfano wa tukio la karibuni la mwananchi aliyechomwa mkuki na kukimbizwa hospitali.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Kiranjeranje, Simba Abdallah, alisema mifugo iliyopo Kilwa kwa sasa inatosheleza na hivyo akashauri watendaji na madiwani kusimamia sheria bila kujenga tofauti kati ya wakulima na wafugaji.

Alisema ipo haja ya kujua idadi ya mifugo iliyozidi na haikuingizwa kwa utaratibu kuondolewa na kurejeshwa ilikotoka.



Afisa Msimamizi Mkuu wa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Edwin Iwato,(kushoto) akitoa elimu ya taratibu za forodha zinazotumika kuwahudumia wafanyabiashara wa kati na wadogo wanaotumia kituo cha huduma kwa pamoja mpakani Sirari. Elimu hiyo imetolewa kufuatia kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango inayoendelea mkoani Mara. (Picha na TRA).

# 'Sayansi itatue uhaba wa maji utokanao na mabadiliko tabianchi'

Na Lucy Ngowi

WANASAYANSI nchini wameshauriwa kutatua changamoto ya maji inayowakabili wanawake kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (Costech), Dk Philbert Luhunga alisema hayo wakati akifungua Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Wanasayansi Duniani yenye kaulimbiu inayohusu changamoto ya upatikanaji wa maji.

Luhunga alisema sayansi ndio ufumbuzi muhimu wa changamoto ya maji nchini inayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

"Dunia inapitia kwenye changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, matokeo yake yanaathiri wanawake na vijana wa kike na sayansi inaweza kusaidia kutatua changamoto hii," alisema.


Aliongeza kuwa wanawake ni waathirika wakubwa wa mabadiliko hayo kuliko wanaume kutokana na shughuli mbalimbali za kijamii zinazohitaji maji safi na salama huku mfumo ukiwafanya wao ndio wahusika wakubwa wa kusaka maji ya familia.

Ofisa Utafiti Mwandamizi, Dk Hulda Gideon alisema sayansi ni msingi wa maisha ndiyo inayofanya jamii iwe na afya.

Alisema kama wanawake katika maadhimisho hayo ya sayansi wanapaswa kujua ushiriki wao ni upi katika sayansi.

"Takwimu zinazotolewa zinaonesha kuwa bado ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali upo nchini," alisema na kuwataka wanawake kuwa mabalozi wa masomo ya sayansi shuleni na vyuoni ili wasichana wapende sayansi.

# Tarura yajipanga kufungua barabara zaidi Sikonge



Na Lucas Raphael, Sikonge

WAKALA ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) wilayani Sikonge, mkoani Tabora unatarajia kufungua mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa 1,680 katika maeneo mbalimbali katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Akizungumza na gazeti hili ofisini kwake jana, Meneja ... wilayani humo, ... kilometa 922.7 zilizohakikiwa na kutangazwa kwenye gazeti la serikali.

Alisema kilometa 148 za barabara zimepimwa na kuwekwa katika mapendekezo ya uhakiki ili ziweze kuongezwa katika mtandao huo na barabara nyingine bado hazijaingizwa katika mfumo huku akibainisha kuwa upitikaji wa barabara zote ni wa wastani.

Alifafanua kuwa hadi sasa wamejenga kilometa 3.1 za lami katika halmashauri hiyo, kilometa 262.88 za changarawe na ... alisema wanatarajia kuongeza barabara za lami hadi kufikia kilometa 3.5, changarawe kilometa 328 na za udongo zitapungua hadi kubaki kilometa 581.

Kaselwa aliishukuru serikali kwa kuwaongezea fedha za matengenezo ya barabara kutoka bajeti ya awali ya Sh milioni 829.8 hadi kufikia Sh bilioni 4.19.

"Tunaishukuru serikali kwa kututengea Sh bilioni 4.19 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya barabara na matumizi ya ofisi, hii bajeti ni mkombozi kwa wananchi wa Sikonge kwa kuwa itawezesha barabara nyingi ...

Alifafanua kuwa ongezeko hilo kuwa ni Sh milioni 820 za matengenezo ya kila mwaka, Sh milioni 500 za majimbo, Sh bilioni moja za tozo na Sh bilioni 1.8 za matengenezo maalumu ya barabara inayounganisha Kata ya Nyahua na makao makuu ya wilaya.

Kaselwa alieleza kuwa jumla ya mikataba minne imesainiwa na wakandarasi kwa ajili ya matengenezo ya barabara 18 kupitia fedha za Mfuko wa Barabara na mikataba mingine mitano kwa ajili ya matengenezo ya barabara 16 kwa kiwango cha changarawe

Scanned with CamScanner

UHIFADHI

# Mgogoro Ngorongoro pasua kichwa

Waandishi wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz





Baadhi ya mifugo ikipata chakula katika eneo la Ngorongoro. Picha na maktaba

**Takwimu**

**100,000**

Idadi ya watu wanaokadiriwa kuwapo katika hifadhi ya Ngorongoro hivi sasa.

Dar es Salaam. Joto la mgogoro wa eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), limezidi kupanda kutokana na kuongezeka kwa shinikizo la kuitaka Serikali iwaondoe wafugaji wa kijamii ya kimasai ambao idadi yao imekuwa ikizidi kuongezeka siku hadi siku na kutishia uhifadhi wa wanyama katika eneo hilo.

Tayari kuna msuguano mkubwa juu ya hatima ya eneo hilo kutokana na madai kuwa baadhi ya watu wenye idadi kubwa ya mifugo wamewaajiri wafugaji wa kimasai watunze mifugo hiyo katika eneo hilo na hivyo kutishia uhai wa wanyama na mazingira.

Inadaiwa wamiliki hao wa mifugo wamekuwa wakitumia fedha zao kuendesha harakati za kuzuia watu kuondolewa kwenye eneo hilo wakihofia endapo hatua hiyo itatekelezwa watapoteza mifugo yao au mifugo hiyo itakosa malisho ya uhakika wanayoyapata hivi sasa.

Kuna baadhi ya watu wanaotaka wafugaji wa kimasai waendelee na shughuli zao kwakuwa ni sehemu ya vivutio duniani huku wengine wakitaka waondolewe ili kuinusuru hifadhi hiyo.

Hata hivyo Mwananchi lina taarifa kuwa huenda mgogoro huo ukapatiwa dawa na Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa anayetarajia kufanya ziara katika eneo hilo na kuzungumza na viongozi na wakazi wa Loliondo na Ngorongoro.

Siku chache zilizopita akiwa bungeni Waziri Mkuu alisema anatarajia kufanya ziara hiyo baada ya kufanya mazungumzo na viongozi wa mkoa wa Arusha pamoja na wale wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Inakadiriwa kuwa wafugaji wa Kimasai wamekuwepo eneo la Ngorongoro na Loliondo mkoani Arusha tangu miaka ya 1700 na hata kabla ya hapo inaelezwa kuwa baadhi ya wafugaji walikuwa wakiishi kwenye hifadhi za wanyama.

### Udhibiti wa watu

Agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kutaka watendaji wa Serikali na taasisi zake kuangalia eneo la Ngorongoro lilifanyiwa kazi na mamlaka zilizo chini yake ikiwemo NCAA iliyoanza kudhibiti ongezeko la watu lakini hatua hizo zinachukuliwa kama manyanyaso na uonevu kwa wafugaji wa kimasai.

Tayari kampeni ya kutaka wafugaji waondolewe katika hifadhi hiyo zimezidi kushika kasi kuanzia kwa wanasiasa, wanaharakati, wabunge, vyombo vya habari na kwenye jumuiya mbalimbali za watu wanaojipambanua ni walinda na wahifadhi mazinngira.

Ziara ya Waziri Mkuu ndiyo inayosubiriwa kwa hamu kubwa na wakazi wa maeneo husika ambao watajua mwelekeo wao

### Waeleza matumaini yao

Mkurugenzi wa Shirika la kutetea wanawake na watoto(MIMUTIE) Rose Njilo alisema ziara ya Waziri Mkuu itasaidia kutatua mgogoro wa ardhi na wanataka katika utatuzi huo ulinde haki za wanawake na watoto.

James Moringe Diwani wa CCM Kata ya Alaitole iliyopo ndani ya mamlaka hiyo, alisema mgogoro uliopo Ngorongoro ni wa kutengenezwa kwa lengo la kuonyesha jamii ya kimasai ndio tatizo.

Mwenyekiti wa baraza la wafugaji Ngorongoro, Edward Maura alisema ziara ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa itaanika ukweli na wanaamini tatizo ni uongozi wa Ngorongoro kushindwa kusimamia mamlaka hiyo.

Mhadhiri Mwandamizi wa Sheria, Chuo Kikuu Cha Tumaini Makumira Dk Elifuraha Laltaika alisema wanataka mgogoro wa Loliondo umalizwe kwa maridhiano na mazungumzo ya pande zote.

Laltaika alisema ni muhimu mazungumzo ni muhimu kwani

Sheria iliyounda mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro ya mwaka 1959 inatambua uwepo wa jamii ya kifugaji Ngorongoro.

> “Jumapili iliyopita nilianza kazi hiyo kwa kukutana na uongozi wa Mkoa wa Arusha, nimewasikiliza, nimekutana na Wizara nimewasikiliza. Hatua iliyobaki ni kwenda. Nitafanya mikutano na wananchi wa Ngorongoro, nitafanya mikutano na wananchi wa Loliondo.
>
> Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa

Mwenyekiti wa viongozi wa mila Ngorongoro,Metui ole Shaudo alisema mazungumzo pekee ndio yataleta mwafaka kwa kuwa baada ya kuitunza hifadhi hiyo kwa miaka 60 leo wanaonekana sio watu muhimu.

Shaudo ambaye aliwahi kuwa mwenyekiti wa CCM wilaya ya ngorongoro na mjumbe wa bodi ya mamlaka ya hifadhi Ngorongoro, alisema hawana mpango kuhama Ngorongoro.

Kiongozi huyo akiwa bungeni siku chache zilizopita aliiagiza Wizara ya Maliasili na Utalii, kutoa semina kwa wabunge ambayo ilifanyika jana bungeni ili wawakilishi hao wa wananchi wajue kwa kina kiini cha mgogoro na kutoa mapendekezo ya njia bora ya kuutatua.

### Bungeni moto

Baadhi ya wabunge waliochangia taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022 walishauri wafugaji hao waondolewe hifadhini kwakuwa baadhi yao wanatumika kuhudumia mifugo ya matajiri wasioishi eneo hilo.

Akichangia mjadala huo, Mbunge wa Mtwara Mjini, Hassan Mtenga ameishauri Serikali iwaondoe kwa nguvu kwa Wamasai katika eneo hilo.

“Kama kule Mtwara wakati watu wanagoma gesi iondolewe mpaka wajue watafaidikaje, mlipeleka vifaru vya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, mkapeleka ma buldoser na vitu vingine kwamba iwe keki ya Taifa ili kila mmoja anufaike, tunaogopa nini? Au kwa sababu kuna matajiri? Kama mling'ata jongoo Mtwara, ng'ateni hayo majongoo sehemu nyingine.

Hata hivyo hoja hiyo ilipingwa na Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka aliyetetea kuwepo kwa wafugaji wa kimasai.

“Wamasai hawa wamekuwa waungwana kwa uhifadhi. Kama kuna kabila lililoonyesha uhifadhi na kuishi na wanyama katika eneo moja bila kuwadhuru ni tarafa ya Ngorongoro. Wananchi hao hao walitoa ardhi yote ya Serengeti, walitoa ardhi yote ya Tarangire, walitoa ardhi yote Ngorongoro, yote ya Manyara,” alisema Ole Sendeka.

### Chimbuko la Wafugaji ndani ya Ngorongoro

Akichangia mjadala wa mgogoro wa Ngorongoro katika mtandao wa Twitter, Makamu Mwenyekiti wa Chadem anayeishi nchini Ubeligij Tundu Lissu alisema, wafuga wamekuwepo kwenye hifadh za wanyama kwa zaidi ya miaka 7000.

Lissu aliyewahi kufanyi utafiti eneo hilo mwaka 199 alisema Wamasai wenyew wamekuwepo hapo tang karne ya 18 (miaka ya 1700).

“Kama wangekuwa ni wah ribifu wa mazingira msingek ta mnyama hata mmoja kati eneo hili,” alisema.

Hata hivyo, alisema baa ya kuja kwa Wakoloni W rumani na baadaye Waing eza, ndipo walipoanza kuw vikwazo.

“Kwa Tanganyika, u dhi ulianza na Wajerumar baadaye wakaja Wainge Mwaka 1921, Ngorongoro tangazwa kuwa eneo te la wanyamapori. Hata h Wamasai waliachwa hifadhi wakiishi na wanya

“Mwaka 1930, uw ukapigwa marufuku, bado wenyeji hawakuor ni tatizo”

**Taarifa hii imeandal Elias Msuya, Daniel na Mussa Juma.**

ZAIDI >

## Ukimya wa watendaji wamshtua Rais

Akihutubia baada ya kuapisha viongozi aliowateua katika Ikulu ya Dar es Salaam Aprili 6, 2021, Rais Samia Suluhu Hassan, alionya kuhusu ongezeko la watu katika eneo la Mamlaka ya Ngorongoro.

“Utalii, Ngorongoro inapotea. Tulikubaliana kwamba ni eneo la aina yake, kwamba watu na wanyama wakae pamoja, lakini sasa watu wanaongezeka.

Tulipoingia kwenye huu mkataba watu walikuwa 9,000 lakini sasa wapo 60,000? 90,000 mpaka 100,000. “Mamlaka na Wizara mpo mnawaangalia tu, maeneo ya Ngorongoro yanachukuliwa mmekaa kimya, Watu sasa hivi wamefikia 100,000 wanyama watazidiwa tu,” alisema Rais Samia.

Alisema pia Ngorongoro inavamiwa na mimea vamizi na kusababisha wanyama wapotee. “Kuhamisha watu sijui mtafanyaje, lakini kama wameshaingia 100,000 wasiendelee kuingia zaidi.”



Scanned with CamScanner